MUHTASARI WA MKUTANO WA KIMATAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA HUDUMA YA UHAMISHAJI NAMBA YA SIMU YA MKONONI (MNP):

(15 - 16 NOVEMBA 2012, DAR ES SALAAM TANZANIA)

Na: TCRA

1.0 Utangulizi

Kuhama na namba katika mawasiliano ya simu inamaanisha uwezo wa kumbadilisha mtoa huduma, huduma au eneo bila kubadilisha namba yako ya simu. Kwa hiyo, hii inamaanisha kuwa Kuhamia Mtandao Mwingine wa Simu bila Kubadili Namba ya Simu ya Mkononi (MNP) ni huduma ambayo inaruhusu watumiaji kubakia na namba zao wakati wa kubadilisha kutoka kwa mtoa huduma mmoja wa simu ya mkononi kwenda kwa mwingine.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliandaa na kufadhili Mkutano wa Kimataifa wa Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi (MNP) ambao uliandaliwa na BSP Media Group UK. Warsha hiyo ilifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Mlimani City jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 15 hadi 16 Novemba 2012. Lengo la Mkutano huo wa tano wa Kimataifa wa Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi nchini mwetu ilikuwa kuwezesha jukwaa la kubadilishana uzoefu kama mchakato wa maandalizi kuelekea uzinduzi unaotarajiwa wa Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi nchini Tanzania.

Ufunguzi wa mkutano huo ulifanywa na Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Profesa Makame M. Mbarawa (Mb) ambaye aliwahimiza washiriki wanapojadili masuala hayo muhimu ya MNP, kuhakikisha pia kuna masuluhisho mengine muhimu yanayohusiana kama vile uchaguzi wa mtandao wa kutumia kwa mawasiliano ya simu ya kimataifa (Carrier Selection) na Rajisi Kuu ya Namba Tambulishi (CEIR) katika tasnia ya simu ya mkononi yanatekelezwa kwa wakati.

Mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki wapatao 100 na wawezeshaji kutoka TCRA (Tanzania), Communication Commission of Kenya (Kenya), Number Portability ya Afrika Kusini, Caughill-Palitz International Ltd, Laurasia (Uingereza), Reforcia (Uswidi), Rabion Consultancy (The Netherlands), Porting XS, Mediafon (Lithuania), Telcodia na Interconnect Communications Consulting (Uingereza).

Washiriki wengi walitoka kwa wadau muhimu wa TEHAMA nchini Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Tanzania. Ufuatao ni Muhtasari wa Warsha.

2.0 Warsha:

2.1 Yaliyozingatiwa:

i. Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi ni jukumu nyeti na litatekelezwa mara moja tu, kwa hivyo ni muhimu kulifanya wakati huu wa kwa mara ya kwanza;

ii. Jukumu la Mdhibiti katika kuhakikisha utekelezaji na usimamizi wa MNP unafanikiwa na Usimamizi: kwa:-

A. Kuweka mfumo mzuri na wenye ufanisi wa kuhama:

(i) Rahisi, Haraka, Nafuu, ya kuaminika

(ii) Weka kanuni zilizo wazi kwa ajili ya ushindani wenye haki

B. Kuwaunganisha watoa huduma kwa pamoja;

(i) Kuyatatua matatizo ya kiufundi, kimchakato na kibiashara

(ii) Kutoa mwongozo wa utekelezaji na maelekezo.

C. Kuwatetea Wateja kwa;

(i) Kuuelimisha umma kuhusiana na MNP

(ii) Kuanzisha ujumbe wa mawasiliano fungamanifu na yenye ufanisi

iii. Kuna nchi za Afrika (Kenya, Ghana, Afrika Kusini, Moroko na Misri) ambazo tayari zimetekeleza MNP, na nyingine ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

iv. Utekelezaji wa MNP unaweza kuonekana kuwa wa gharama kubwa na hauwezi kuthibitishwa kwa njia ya uchambuzi wa kawaida wa Faida ya Gharama (Cost Benefit Aanalysis). Kwa hiyo gharama ya utekelezaji wa MNP inapaswa kuzingatiwa kama gharama ya kufanya biashara na Watoa huduma;

v. Kwamba, wakati MNP itakapotekelezwa vizuri, inaweza kufanya mchakato wa kuhama kuwa rahisi kama kumsajili mtumiaji mpya.

2.2 **Kutambuliwa**

i. Ukweli kwamba namba za simu zimekuwa za binafsi kwa wamiliki kama njia ya kuwasiliana, hivyo ni muhimu kwamba wanaweza kuhifadhi namba zao za kipekee wakati wanafanya uchaguzi wa mtoa huduma yupi amtumie;

ii. Kwamba MNP ni fursa na watoa huduma wanaweza kupata mapato kwa kiasi kikubwa;

iii. Kwamba, MNP haiathiri hisa za soko au kusababisha bei yenye ushindani lakini inaweza kusababisha athari mbaya ikiwa washindani wataanza kugombania bei;

iv. Hitaji la kuwa na gharama nafuu ya Uhamishaji Namba nchini Tanzania kupitia

uwekaji wa viwango unaofaa.

v. Uhitaji wa elimu endelevu na uelewa kwa watumiaji ili watambue mchakato wa MNP na hivyo kuwa na ujasiri katika kuhama.

2.3 Mambo ya Kujifunza:

i. Ofisi ya MNP Tanzania itaendeshwa na mtu huru anayeaminika na mwenye leseni;

ii. Kwamba Tanzania imechagua utaratibu wa kuhama na namba wa "Direct Routing All Call Query" wenye kuruhusu mtoa huduma kusimamia namba zao wenyewe, kuruhusu huduma kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine kupitia kanzi data zilizopo kwa watoa huduma ambazo huifadhi nakala ya kanzi data kuu na ni nyumbufu kwa kuongeza au kufutwa kwa watoa huduma;

iii. Mdhibiti yuko makini zaidi kutekeleza wa MNP nchini Tanzania na mchakato huu umehusisha michakato ya ushauri hadi sasa katika utungaji wa sheria na kanuni ambazo zinafuatwa kwa kutoa leseni kwa Msimamizi, usimamizi wa programu za MNP na kutekeleza shughuli na kufuata na utekelezaji;

iv. Kwamba kuna nchi nyingine kama Afrika Kusini ambako ofisi ya MNP inamilikiwa kwa pamoja na Watoa huduma wa simu za mkononi kupitia kampuni yenye kumiliki hisa sawa miongoni mwao;

v. Watoa huduma wanahitaji pendekezo la kushindana la thamani ili kuvutia walipaji na kifungu cha MNP na mchanganyiko wa Bidhaa na Huduma zinazofaa zinazolengwa kwa sehemu zinazohusika.

vi. Watoa huduma wanahitaji kuanzisha au kuimarisha Programu za Kulinda Mrabaha;

vii. Watoa huduma wote pia watakuwa wapokeaji wa watumiaji kutoka kwa washindani kwa hiyo MNP haipaswi kuonekana kama tishio badala yake inapaswa kuwa fursa;

viii. MNP ni zana ambayo hutumiwa na Mdhibiti ili kukuza ushindani kuboresha huduma na kusababisha hamasa ya ubunifu;

ix. Ili MNP ifanikiwe, bei za huduma tofauti kati ya simu zinazopigwa ndani ya mtandao (the on-net) and simu zinazopigwa kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine (off-net) inahitaji kuachwa;

x. Katika baadhi ya nchi hasa Ghana, mteja halipii ada ya porting. Gharama ya porting hubebwa na mtandao mpokeaji;

xi. Kanuni za MNP nchini Tanzania zinaainisha *Njia, Ufumbuzi na Masharti* ya Uhamishaji Namba.

2.4 Ilipendekezwa:

i. Maelezo ya Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi nchini Tanzania yanahitaji kutolewa ili kuwaongoza watoa huduma;

ii. Watoa huduma nchini wanatekeleza majukumu yao ili kuhakikisha Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi unatekelezwa na kusimamiwa kwa ufanisi nchini Tanzania kwa kutumia Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta (Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi), 2012.

3.0 Hafla ya Kufunga Mkutano

Sherehe ya kufunga mkutano huo zilihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Dkt. Florens Turuka ambaye alisisitiza kuhusiana na hotuba ya Waziri.

Kwa upande wake kama serikali, Katibu Mkuu alithibitisha kuwa atatumia changamoto zilizoainishwa wakati wa hafla hiyo kama fursa za kupanga vizuri na kuzindua MNP nchini Tanzania kwa kutumia kanuni ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta (Uhamishaji Namba ya Simu ya Mkononi) ambayo inataja *Njia, Suluhisho na Masharti ya Uhamishaji* Namba ya Simu ya Mkononi. Kwa kumalizia, aliwashukuru Waandaaji na Mdhamini Mkuu kwa tukio hilo la kimataifa.